Biblia inaweza kubadilisha maisha yako. Kutenga muda kila siku ili kusoma Biblia hata kwa kiasi kidogo ni jambo la kwanza kwa Mkristo pamoja na kujitoa katika Kanisa. Tumeandaa njia kadhaa za kuchagua ambazo zinaweza kuwasaidia vijana kulishika Neno la Mungu:

1. Soma Agano Jipya kwa mwaka mmoja ukitumia mpango wetu uitwao Soma Agano Jipya kwa Mwaka Mmoja – Hii ni njia nzuri ya kukuza ufahamu wa ujumbe wa Kikristo, kuongeza kina cha imani na kukutana na Yesu. Washiriki katika huduma hii watasoma zaburi moja na sura moja ya Agano Jipya kila siku. Baada ya kumaliza kusoma kila siku, jiulize wewe mwenyewe: 1) Maandiko haya yananifundisha jambo gani kuhusu Mungu? 2) Yananifundisha nini kuhusu watu wengine? 3) Yananifundisha kitu gani kuhusu maisha yangu mwenyewe? Tafakari maswali haya peke yako, au na rafiki au kikundi.

2. Soma Biblia ya Mwaka Mmoja – Biblia ya Mwaka Mmoja ina masomo yaliyochaguliwa toka kwenye Biblia kwa ajili ya kila siku, ikitumia masomo kutoka Agano la Kale na Agano Jipya. Vifungu vigumu zaidi, vinavyochosha na vyenye ukatili vimeachwa. Hii ni njia bora zaidi ya kumsaidia mtu anapopata uzoefu wa kusoma Biblia mara kwa mara. Katika kila hitimisho la somo, jiulize mwenywe: 1) Masomo ya leo yananifundisha nini kuhusu Mungu? 2) najifunza nini kuhusu watu wengine? 3) Yananifundisha kitu gani kuhusu maisha yangu mwenyewe? Tafakari maswali haya peke yako, au na rafiki au kikundi. Biblia ya Mwaka Mmoja ina masomo yaliyochaguliwa toka kwenye Biblia kwa ajili ya kila siku, ikitumia masomo kutoka Agano la Kale na Agano Jipya. Tumia *Google* kutafuta: Biblia ya Mwaka Mmoja ili pia upate kuchagua njia nyingine zaidi zinazopatikana kwenye mtandao wa *Amazon.com*

3. Tumia nguvu ya teknolojia na kupakuwa kimtandao Biblia bila malipo – Jaribu kupakuwa Biblia kwenye mtandao na kuiingiza kwenye *iPad*, *iPhone*, *Kindle* au *Nook*. Uwe na Biblia yako wakati wote. Mitandao ya *YouVersion.com* na *bible.com* inatoa taratibu nyingi za usomaji wa Biblia kwa njia ya kusoma Biblia kwa mwaka mmoja huku ikikupa utararibu wa kukuwezesha kujifunza masomo ya imani, upendo na mambo mengine. Tovuti hizi pia zina vipakuzi kwa ajili ya simu za kiganjani kama vile *smart phone*, *iPad*, *Blackberry* na simu za *Android* [kama vile *Sumsung Galaxy Appeal*].

Tovuti ya *Oneyearbibleonline.com* inatoa mpango wa usomaji ambao umegawanywa katika masomo ya kila siku yakiwa na kifungu kutoka Agano la Kale, Agano Jipya, Zaburi, na Mithali. Tovuti ya *Biblegateway.com* ina Biblia nzuri nyepesi kufunguka tena yenye njia nyingi za kukuwezesha kupata unachokitaka. Tovuti nyingine ni *Bibleresources.bible.com* hii ina mambo mengi mazuri. Tovuti za *Amazon.com*, *Zondervan.com*, na *BN.com* zinatoa Biblia za aina mbalimbali na vipakuzi kwa ajili ya simu za kiganjani na vifaa vya kusomea kama *Kindles*, *Nook Readers*, *Smart phones*, *Blackberry*, simu za *Android*, pia Biblia iliyoigizwa kwa Sauti ya *NIV* na *CD*.

4. Sikiliza Biblia – Siku hizi kuna vifaa vingi vinavyoweza kukuwezesha kusikiliza Biblia unapoendesha gari kuelekea shuleni, unapotembea na mbwa wako, unapofanya mazoezi, unaposafiri au ukiwa umepumzika nyumbani au kitandani. Hili ni jambo jema sana kwa wale wenye kawaida ya kusikiliza zaidi kuliko kusoma. Unaweza kusikiliza Biblia katika tafsiri mbalimbali kwa njia na programu za kimtandao kama hizi: *Audio.com/Bible*, *listenersbible.com*, *BibleGateway.com*, *YouVersion.com* au *www.faithcomesthroughhearing.com.*, ambazo zinakupa programu za kusikiliza Biblia katika lugha 692. Unaweza kusikiliza Agano Jipya lote kwa dakika 28 kila siku kwa siku 40.

5. Kukariri Maandiko – Kikariri Maandiko ni njia kuu ya kukuza imani yako na kuongeza ufahamu wako wa Biblia. Tunapokariri kitu, tunaweza kukikumbuka, tunaporudia kukisema kitu kile kile basi hali hiyo inatuwezesha kuwaza, kufanya maamuzi na kueleza yale tunayoyaamini. Kukariri Biblia husaidia kutujenga katika tabia na utu. Pia kuna tovuti iitwayo *bibleminded* ambayo inakuwezesha kukariri vifungu wewe mwenyewe au kwa kufuata njia moja wapo kati ya kadhaa zilizowekwa. Tunashauri usome sura moja ya Biblia kwa siku na kuwekea alama kifungu kimoja cha kukariri. Kiandike kufungu kwenye karatasi au kadi unayoitumia kuwekea alama kwenye Biblia. Tumia dakika kadhaa ukijaribu kukariri hicho kifungu. Chukua karatasi hiyo uwe nayo, fanya mazoezi ya kurudiarudia kusema kifungu kwa siku nzima. Mwisho wa siku, utakuwa umeshakikariri kifungu husika. Vile vifungu uvipendavyo vipitiepitie aghalabu mara moja kwa wiki.

6. Soma Mkusanyiko wa Ujume wa Eugene Petersen – Mkusanyiko wa Ujumbe ni toleo lililotafsiriwa mahsusi kwa vijana na Eugene Petersen na ameuza nakala nyingi. Ni utangulizi mzuri wa Biblia kwa wale wanapata shida kusoma Maandiko ya Biblia yenyewe kama yalivyo; pia ni toleo linalofanya masimulizi na vifungu vya Biblia kugusa maisha halisi tena kwa upya kabisa. Baada ya kusoma toleo hili, unaweza kusoma Biblia wewe mwenyewe. Tembelea tovuti hii: *www.messagebible.com* ikiwa unataka kuagiza nakala yako.

7. Soma Toleo la Masimulizi kwa ajili ya Vijana – Mfululizo wa mkusanyiko wa masimulizi ya Biblia wa Zondervan umewekwa pamoja katika mtindo wa mtiririko wa mmoja unaofanana na kitabu cha hadithi. Maelezo marefu ya sharia za vyakula, nasaba na sehemu za Biblia zinazojirudia zimeachwa kabisa. Baada ya kusoma toleo hili, utakuwa tayari kusoma Biblia yote wewe mwenyewe. Tembelea tovuti hii: *www.thestory.com* ili kuagiza nakala yako.

8. Soma Biblia yote kwa Mwaka – kwa vijana wenye imani iliyokomaa ambao wameshasoma Agano Jipya lote, Mkusanyiko wa Ujumbe, Toleo la Masimulizi ya Biblia kwa Vijana au Biblia ya Mwaka Mmoja, tunawashauri wasome Biblia yote wakitumia ule mpango wa Soma Biblia kwa Mwaka Mmoja, ambao unaweza kuupakua toka kwenye tovuti yetu ya: *www.thecenterforbiblicalstudies.org*. Mwisho wa kila somo, jiulize mwenyewe: 1) Ni jambo gani lililonishangaza zaidi katika usomaji wa Biblia wa leo? 2) Je, ni kwa namna gani maandiko haya yamenipa changamoto au kuthibitisha imani yangu? 3) Je, ni kwa namna gani Mungu ananihimiza kukuwa kiimani kutokana na somo nililosoma?

9. Soma Injili ya Luka na Kitabu cha Matendo – Ikiwa kusoma sehemu kubwa ya Biblia kunakupa changamoto kubwa, anza usomaji wa polepole. Soma Luka, injili ambayo imejaa habari za maisha na huduma ya Yesu na imejaa mifano mikubwa. Jambo hili litakupa utangulizi mkubwa wa maisha ya Yesu. Kitabu cha Matendo ya Mitume kitakufundisha namna Wakristo wa kwanza walivyoanza kuueneza ujumbe na upendo wa Yesu.

10. Jiunge na Mtaala wa Biblia uliopo au Anzisha Wakwako – Biblia hueleweka vizuri zaidi unaposoma na kujifunza pamoja na wengine. Kiini cha imani siyo kuwa na majibu yote bali kuuliza majibu sahihi. Mitaala ya Biblia inatusaidi kuwa na maswali mazuri na kujifunza toka kwa wengine. Kama hakuna mtaala wa Biblia kanisani kwako, anzisha nyumbani kwako, shuleni au kanisani. Waalike marafiki kujiunga na mtaala wako. Anzeni kwa kusoma Injili. Kisha mnaweza kusoma Kitabu cha Matendo na Nyaraka za Paulo kwa Warumi na Wakorintho. Kwa upande wa Agano la Kale, anza na Mwanzo na Kutoka.

Shuhuda

Changamoto ya Biblia inaendelea vizuri sana. Sijafaulu kusoma kiasi kikubwa kwa siku kwa kuwa shule imefungua, lakini nahakikisha kuwa siku zote nasoma walau kiasi kidogo kwa siku. Lililo la muhimu zaidi ni kwamba usomaji wa Biblia limekuwa jambo linalotunza imani yangu katika akili yangu kwa karibu muda wote… Pia, naweza kusema kuwa ni kitu ninachopenda kuendelea nacho. Siyo kwamba ninauhakika kwamba nitamaliza tu, bali pia ninauhakika kwamba mara nikimaliza, nitarudia sehemu kadhaa za Biblia na kuzisoma tena. Ninauhakika kuwa usomaji wa biblia wa kila siku utabaki kuwa sehemu ya ratiba yangu ya kila siku. Nashukuru kwa kuniwezesha kuifahamu Changamoto hii; kimekuwa kitu cha baraka kubwa katika maisha yangu. – **Allie** (umri17)

Changamoto ya Biblia kwa Vijana inanipa fursa ya kuisoma Biblia kwa mpangilio. Pamoja kuwaza mambo ya chuo, na ratiba yenye shughuli nying za masomo, kuwa na muhtasari unaoniongoza kuisoma Biblia yote ni ni msaada mkubwa sana kwangu." – **Alec** (umri 17)

Ninaendelea kusoma – na kutumia kile ninachokisoma. Jana usiku tu, katika Mkutano wa Vinaja, niliweza kutumia nukuu ya Biblia kutoka Injili ya Mathayo tena kwa wakati muafaka; na kwa muda mfupi tu tulipata vijana 14 wa darasa la 6 – 8 waliozingatia swali tulilolijadili. "Kwa hiyo wa mwisho atakuwa wa kwanza, na wa kwanza atakuwa wa mwisho." Ilikuwa sawa kabisa kwa kadri walivyokuwa akifikiri maana ya nukuu hii na jinsi ilivyohusiana na maisha yao. Tulikuwa na majadiliano ya kina kwa dakika kumi hivi ambapo hakuna aliyembeza mwingine alipozungumzaa (hili lilikuwa jambo la kukumbukwa katika kikundi chetu cha Vijana) - **Jim** (kiongozi wa kikundi cha vijana)

Kabla ya kuanza Changamoto ya Biblia, hapa tunakuletea mambo kadhaa ya kufikiria kabla ya kuanza:

Nianze lini Changamoto ya Biblia?

Unaweza kuanza Changamoto ya Biblia wakati wowote utakavyo. Tarehe 1 Januari ni tarehe nzuri ya kuanza, kama unataka kufanya uamuzi wa kiroho kusoma baadhi ya sehemu za Biblia kila siku kwa mwaka ujao. Vinginevyo, anza katika siku yoyote upandayo. Somo sehemu kidogo tu ya Biblia kila siku hali ukimuomba Mungu, liache Neno la Mungu lipenye moyoni mwako, akilini na nafsini. Tovuti yetu: *www.thecenterforbiblicalstudies.org* inatoa maelekezo mengi ya kukusaidia wewe.

Tafsiri gani ya Biblia yafaa niisome?

Tunawatia moyo vijana [watumiao lugha ya kiingereza] kusoma Biblia iitwayo *Spark Bible*, au Bibli ya *New Revised Standard Version*. Hii ni Biblia nzuri sana, tafsiri inayoweza kusomeka kwa urahisi tena ina maelezo na maswali ya kumsaidia msomaji. Tembelea tovuti hii: *http://www.wearesparkhouse.org/bibles/* ili uweze kuagiza nakala yako. Pia tunapendekeza tafsiri ya Biblia iitwayo *Common English Bible*. Ina faharasa, ni nyepesi na inayobebeka kwa urahisi. Mnaosoma Biblia kwa mara ya kwanza epukeni ile tafsiri ya Biblia iitwayo King James, kwa sababu ina changamoto kubwa zaidi kuisoma. [kwa msomaji wa Kiswahili usome Biblia Takatifu ya Kiswahili yenye Itifaki ya mwaka 1997 (*The Holy Bible in* Kiswahili *Union Version with Concordance 1997*) ambayo ni nzuri kwa mtaala wa Biblia, au unaweza kutumia tafsiri ile ya Kiswahili cha kisasa. Kumbuka kutumia tafsiri za zamani kama *Union Version* ya 1952 unaposoma Biblia kwa mara ya kwanza inaweza kuwa kazi ngumu zaidi]

Ni kwa namna gani nashauriwa kuanza kusoma Biblia?

• Kwa kuwa Biblia siyo gazeti, ni bora zaidi kuisoma kwa moyo wa unyenyekevu. Tunasisitiza utaratibu wa kusoma Biblia kwa utulivu kwa sala na maombi, badala ya kuisoma kama jambo la kiakili tu au kama utaratibu wa kitaaluma. Tunakutia moyo uanze kila kipindi cha kusoma Biblia kwa kujiweka mwenyewe mbele ya uwepo wa Mungu wakati unapoanza kusoma Biblia.

• Soma ukiwa na hamu ya kuelewa na kuyafuata mafundisho yaliyomo katika Maandiko ili maisha yako yabadilishwe na Roho Mtakatifu anayefanya kazi ndani yako.

• Tunapenda mapokeo ya kale ya kimonaki ya *lectio divina*, ambapo husoma maandiko, hutafakari, kisha kumuomba Mungu na kumsikiliza majibu ya Mungu kwa kimya kimya. Hivyo tunashauri wasomaji wote wasome Biblia katika hali ya sala na maombi..

• Tunakuhimiza kujisomea asubuhi kwa dakika 20 au 30, ili usomaji wako unaoambatana na maombi ukupe hamasa ya kiroho kwa siku yako yote. Kama huwezi kusoma asubuhi basi usome baadaye, na hasa kama unaweza kujipangia muda fulani wa kusoma kila siku.

• Kama unasoma Agano la Kale, tunakuhimiza kuruka au kusoma kwa haraka maelezo marefu ya nasaba, sheria za vyakula na maelezo mengine yaliyo marefu. Pata wazo la jumla na kuendelea mbele.

• Kujiwekea utaratibu mzuri wa kusoma Biblia kila siku ni muhimu sana kwa siku 21 za kwanza. Baada ya hapo, utakuwa tayari umejijengea tabia njema ya kusoma Biblia.

• Tunakutia moyo uufurahie usoma wako na kujipatia amani na furaha ya rohoni unapoendelea kusoma Neno la Mungu.

• Lengo letu kuu ni kukuwezesha wewe kugundua hekima ya Mungu kwa ajili ya maisha yako ya kila siku na kujenga tabia ya kiroho ya kusoma Biblia kwa maisha yako yote.

Nguvu ya pamoja na kuwafikia wengine ili kupata msaada katika usomaji wa Biblia

• Njia mojawapo ya kuhakikisha kwamba unasoma vifungu vya Neno la Mungu kila siku na kuelewa kile unachosoma ni kuanzisha mtaala wa Biblia nyumbani kwako, kanisani au shuleni na kusoma Biblia na marafiki. Mnaweza kusaidiana, kulizana maswali, kujadili kile mnachokisoma na kushirikishana jinsi Neno la Mungu linavyobadilisha maisha yako.

• Baada ya mwaka au kipindi fulani cha kusoma Biblia pamoja, tunahimiza muandae chakula cha pamoja ili kusherekea mafanikio yenu ya kiroho.

• Kama una maswali kuhusu kile unachokisoma, wasiliana na mchungaji au kiongozi wa vijana katika kanisa lako.

Maisha baada ya Changamoto ya Biblia

• Kama usomaji wa Biblia limekuwa ni jambo la baraka, sasa washirikishe wengine baraka hiyo. Waalike baadhi ya marafiki zako au familia yako kushiriki katika Changamoto ya Biblia.

• Tunawahimiza washiriki waone kwamba kusoma Biblia kila siku ni jambo muhimi sana la kiroho kwa maisha yao yote. Biblia ni kijito cha hekima kisichokauka ambacho kinaweza kutumwagia baraka kila siku katika maisha yetu. Rais John Adams, rais wa pili wa Marekani, alisoma Biblia yote kila mwaka katika maisha yake ya utu uzima na alipata baraka kubwa kwa kufanya hivyo. Tunakutia moyo uifuate tabia hii.

Bwana ataheshimu bidii yako katika kusoma Neno la Mungu. Ikiwa jambo hili la kiroho limegusa moyo wako na kukupa chakula cha kiroho, nakualika uchangie Kituo cha Masomo ya Biblia ili kusaidia kukuza Changamoto ya Biblia ili wengine wanufaike na usomaji wa Neno la Mungu kila siku na kushiriki katika Changamoto ya Biblia. Sadaka yako inaweza kutolewa kwa "*Christ Church Greenwich*" ukieleza ni kwa ajili ya "*The CBS*" na uitume kwenda Christ Church Greenwich 254 E. Putnam Avenue, Greenwich, CT 06830.

Nuru na upendo wa Mungu vikuangazie kila siku,

Mch. Marek P. Zabriskie

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Christ Church Greenwich (Connecticut), na Mwanzilishi wa Kituo cha Masomo ya Biblia na Changamoto ya Biblia.

Ili kujiunga na Changamoto ya Biblia, tafadhari nitumie barua pepe kwa anuani hii:
mzabriskie@christchurchgreenwich
Tofuvi yetu *thecenterforbiblicalstudies.org* inakupa mambo mengi ya kukusaidia.

©